

TANGAZO LA SERIKALI NA. 458 la tarehe 24/6/2022

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,  
(SURA YA 415)

---

## AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 28(3))*

---

AMRI YA NAULI ZA ABIRIA KWA USAFIRI MAJINI, 2022

- Jina 1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Nauli za Abiria kwa Usafiri Majini, 2022.
- Matumizi 2. Amri hii itatumika kwa meli zinazomilikiwa na Kampuni wakati zikisafiri kwenye njia za-
- (a) Mwalo wa Kirumba, Mwanza kwenda Kisiwa cha Godziba;
  - (b) Mwalo wa Kirumba, Mwanza kwenda Gana; na
  - (c) Gana kwenda Godziba.
- Tafsiri 3. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo-  
Sura ya 415 “Sheria” maana yake ni Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;  
Sura ya 212 “Kampuni” maana yake ni Kampuni ya Huduma za Meli iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni;  
“Shirika” maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria; na  
“meli” maana yake ni MV. Clarias, ML. Wimbi na meli nyingine zinazoendeshwa na Kampuni katika Ziwa Victoria.
- Tozo ya nauli 4. Kampuni itakapokuwa ikiendesha meli yoyote, zilizoidhinish ikiwemo MV. Clarias na ML. Wimbi itapaswa-  
wa
- (a) kutoza nauli ya abiria na mizigo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Amri hii;
  - (b) kumtoza mtoto mwenye umri wa kati ya miaka mitano na kumi na moja, nusu ya nauli ya mtu mzima; na
  - (c) kuzingatia masharti ya utoaji huduma ya usafiri kwa njia ya maji yaliyotolewa na Shirika kwa mujibu wa Sheria.
- Masharti ya 5. Kampuni, wakati ikitoa huduma, itazingatia masharti  
huduma yafuatayo:
- (a) haitatoza mzigzo unaoambatana na abiria ambao hauzidi kilo ishirini;
  - (b) haitatoza nauli kwa mtoto mwenye umri chini ya

miaka mitano;

- (c) itaimarisha mikakati ya kimasoko ili kuongeza idadi ya abiria na shehena;
- (d) itawasiliana na wamiliki wa eneo la mwalo wa Kirumba, Gana na Godziba ili kurasimisha maeneo hayo ya kibandari na kuboresha miundombinu kwa usalama wa huduma; na
- (e) itazingatia viwango vya usalama kama vilivyotolewa katika Sheria ya Usafiri Majini na kanuni zake.

Sura ya 165

### JEDWALI

*(Imetengenezwa chini ya aya ya 4(a))*

#### **UKOMO WA NAULI ZILIZOIDHINISHWA**

Njia	Nauli ya Mtu Mzima (TZS)
Kirumba – Godziba	16,500
Kirumba – Gana	10,500
Gana – Godziba	6,000

#### **UKOMO WA NAULI YA MIZIGO**

Bidhaa	Kipimo	Kirumba Cluster Port–Gana/Godziba
Dagaa	kilo 50	4,000
Samaki Wabichi	kilo100	11,500
Samaki Wakavu	Kilo 100	17,500
Mabati	1 Bando	15,000
Sementi	Kilo 50	2,500
Bia/Soda	1 kreti	1,200
Injini	1	20,000
Ngano	Kilo 50	900
Mizigo mingineyo	Kilo 50	4,000

Dar es Salaam,  
17 Juni., 2022

KAIMU ABDI MKEYENGE  
*Mkurugenzi Mkuu*